# *BARUA #00; UTANGULIZI WA MWAKA WA MAFANIKIO 2020/2021.*

Kwako rafiki yangu mwanamafanikio,

Nichukue nafasi hii kukupongeza kwa kuchagua safari hii ya mafanikio, ni wachache mno wanaochagua safari ya aina hii na kujitoa kweli kuweza kufanikiwa.

Pia nikukaribishe twende pamoja kwenye safari hii, kwa miaka kumi ijayo, tutakwenda pamoja, hatua kwa hatua mpaka tuweze kufika kwenye mafanikio makubwa zaidi bila ya kuchoka.

Kwenye SEMINA YA KISIMA CHA MAARIFA 2020 mwanamafanikio mwenzetu Enelisa Mbwile aliuliza mpango wa mafunzo kwa mwaka huu wa mafanikio ni upi, maana kila mwaka wa mafanikio nimekuwa nashirikisha mpango wa mafunzo. Miaka ya nyuma zilikuwa semina mbili za njia ya mtandao, mwaka jana ilikuwa mpango wa KIPATO ZAIDI 2020.

Kwa mwaka huu wa mafanikio, mpango wa mafunzo zitakuwa ni barua nitakazokuwa naandika kila wiki. Barua hizi zitalenga kujibu changamoto mbalimbali ambazo wanamafanikio wanapitia kwenye hatua kubwa wanazochukua ili kufika kwenye mafanikio makubwa.

Kwa muongo huu kila mmoja wetu anakwenda kuchukua hatua kubwa, na hatua hizo zitazalisha changamoto kubwa pia, lazima tuwe na namna bora ya kutatua changamoto hizo ili zisiwe kikwazo kwetu.

Hivyo mpango huu wa BARUA ZA MAFANIKIO, kila wiki tutajadili kwa kina changamoto moja na kuiangalia vyanzo vyake, njia za kuitatua na kuzuia isirudi tena na kuwa kikwazo.

Karibu sana kwenye mfumo huu wa masomo ya BARUA ZA MAFANIKIO 2020/2021 tuweze kujifunza, kuchukua hatua na kufanikiwa zaidi.

Changamoto nitakazoziandikia nitazipata moja kwa moja kutoka kwenye tathmini za mwezi

ambazo kila mwanamafanikio atakuwa anatuma.

## MPANGO WA MUONGO NA MWAKA.

Nilitoa mwongozo wa MWAKA WA MAFANIKIO 2020/2021 ambao utatuongoza wote.

Kwenye mwongozo huo nilitoa maelekezo ya kila mwanamafanikio kutuma mpango wa muongo (2020 - 2030) na mpango wa mwaka (2020/2021) na hatua anazokwenda kuchukua.

Wanamafanikio wapatao 62 mpaka sasa wametuma mipango yao na hatua wanazopanga kwenda kuchukua.

Karibu wote ambao wametuma mipango yao, NDOTO kubwa wanayofanyia kazi ni KUFIKIA UHURU WA KIFEDHA, hivyo tutaambatana pamoja kuhakikisha kila mtu anafikia ndoto hiyo.

Lakini pia kila mmoja ana mpango mkubwa kwa muongo huu, ambapo wengi ni kufikia Ubilionea kupitia njia mbalimbali. Wengi wameainisha vizuri na wengine tunaendelea

kusaidiana kuainisha ili waweze kuwa na namba wanayoifanyia kazi na kujipima kadiri tunavyokwenda.

Wote waliotuma mipango yao wamenipa ahadi ya kuwa pamoja na kujisukuma ili kufikia mafanikio makubwa. Niwaahidi kwamba nitashikilia ahadi hiyo na kuhakikisha kila mtu anafikia mafanikio makubwa aliyojiwekea.

Kama bado hujatuma mpango wako, fuata maelekezo yaliyopo kwenye MWONGOZO WA MAFANIKIO 2020/2021 na tuma mpango ili tuweze kwenda pamoja. Unaweza kupakua mwongozo huo kwa kubonyeza maandishi haya.

## KUFANYA KAZI NA WATU WACHACHE.

Kwa miaka zaidi ya 6 ambayo nimekuwa natoa huduma hii ya KISIMA CHA MAARIFA, nimefanya kazi na watu wengi.

Wengi wamekuwa wanakuja na kuondoka, lakini kuna wachache ambao nimekuwa nao

katika kipindi chote hicho na nimeona wakipiga hatua kubwa mno, hatua ambazo zinanipa moyo sana na kuona kile ninachofanya kinakuwa na mchango mzuri kwa wengine.

Nilichokiona ni wale ambao wanatulia, wanajifunza na kuchukua hatua, hata kama ni kidogo hawabaki vile walivyokuwa. Lakini wale ambao wanakuwa wapo tu, hawajifunzi na hata wakijifunza hawachukui hatua, hawapigi hatua yoyote.

Nimekuwa nachoshwa sana na kuhangaika kufanya kazi na watu wengi, halafu hawaweki uzito kwenye kazi hii kama mimi ninavyoweka. Kila wakati nahangaika na watu ambao hawajisumbui hata kidogo.

Baada ya kufanya tathmini ya kina na kuona nini kinafanya kazi na nini hakifanyi kazi, nimechagua kufanya kazi na watu wachache, wasiozidi 100 kwa kipindi cha miaka kumi ijayo.

Kwa wale watakaopata nafasi hiyo, nitajitoa kwa kila niwezavyo kuhakikisha wanafanikiwa. Tunapofika mwaka 2030, watu wote 100

ambao nimeambatana nao wawe wamefanya makubwa mno kwenye maisha yako, kwa taifa na dunia kwa ujumla.

Hatua ya kwanza ya kuchukua ili upate nafasi hii ni kutuma mpango wako wa muongo na mwaka na kuweka ahadi yako kwamba tutaambatana pamoja katika safari hii.

Ukishanipa ahadi hiyo, mimi sitakuacha nyuma. Yaani hakuna namna nitakuacha nyuma, hata kama utakataa, mimi bado nitaendelea kukomaa na wewe, kwa sababu umenipa ahadi yako na ahadi ni deni.

Hivyo nikukaribishe sana twende pamoja kwenye safari hii, tunaona matokeo mazuri kwa kila anayejifunza na kuchukua hatua, inawezekana hata kwako pia.

## ONGEZEKO LA ADA.

Kwa kuwa hakutakuwa na ongezeko la wanachama na kwa kuwa muda wangu mwingi nitauweka kuhakikisha kila mmoja anafikia

lengo alilojiwekea, kutakuwa na ongezeko la ada ya KISIMA CHA MAARIFA.

Ongezeko hili litakuwa linaendana na kiwango cha ukuaji cha kila mwanachama. Kitakuwa kiasi ambacho kila mwanachama anaweza kukimudu kulingana na hatua aliyopo kwenye ukuaji wake.

Kitu kimoja ambacho nakuahidi ni kwamba hakuna atakayeikosa nafasi ya KISIMA CHA MAARIFA kwa sababu ameshindwa kulipa ada. Kama umejitoa kweli, unajifunza na unachukua hatua, nitakusaidia uweze kukuza kipato chako na uweze kumudu ada yako bila ya tatizo lolote.

## KARIBU TUSAFIRI PAMOJA.

Rafiki yangu mpendwa, ahadi yangu kuu kwako ni hii; kazi yangu kubwa na ya kwanza ni wewe. Mafanikio yako ndiyo mafanikio yangu, nimejitoa kuhakikisha unafanikiwa kweli, hivyo nitumie kadiri uwezavyo.

Kwa wale wote waliojitoa tusafiri pamoja nitakufuatilia kwa karibu sana, kuna wakati

utaona kama nakusumbua, lakini lengo langu ni kukuona unapiga hatua. Ninafanya hivyo kwa nia njema kabisa na nikiwa na upendo mkubwa sana kwako.

Karibu sana twende pamoja, kama bado hujachukua hatua nilizoainisha, fanya hivyo, miaka hii kumi itakwenda kuwa ya kufanya makubwa, haitakuwa rahisi, lakini mwisho wa siku tutafika pale ambapo wengine wameshindwa kufika.

Hili naliamini ndani ya moyo wangu na sina shaka yoyote, kama tutaambatana pamoja, nina uhakika utafika mbali mno.

Ninachoomba kwako ni rahisi sana, jifunze, chukua hatua na toa mrejesho.

Kila mwezi tuma tathmini ya hatua ambazo umechukua kwenye mwezi husika na matokeo ambayo umeyapata.

Unapokuwa na changamoto au kuhitaji ushauri, wakati wowote tuwasiliane.

# NJIA KUU ZA MAWASILIANO.

Njia kuu ya mawasiliano ni barua pepe, ambapo nimeshaelekeza kutumia email moja ambapo mawasiliano yote yatafanyika. Email ambayo utaitumia kuwasiliana na mimi ni kochamakirita@gmail.com Usitumie email nyingine yoyote.

Kwa simu namba itakayotumika kwa mawasiliano ni 0755 953 887 kwa ujumbe au kupiga. Wasap ni namba 0717396253.

Mawasiliano ni vyema yakaanzia kwenye email kwa sababu ndiyo namna nzuri ya kutunza mfululizo wa mawasiliano na pale itakapohitajika tutawasiliana kwa simu.

# MAONI, SHUHUDA NA MASWALI.

Karibu kwa maoni, shuhuda na maswali kuhusu barua hii.

Kama kuna mahali hujaelewa na ungependa ufafanuzi zaidi basi karibu uulize swali.

Kama kuna eneo unaweza kuongeza maoni zaidi karibu pia.

Na kama una ushuhuda wa namna umewahi kufanyia kazi yale uliyojifunza kwenye barua hii, karibu utushirikishe matokeo ambayo uliyapata.

Maoni, maswali na shuhuda viwekwe moja kwa moja kwenye kundi la KISIMA CHA MAARIFA wasap.

Nikutakie kila la kheri katika kufanyia kazi haya uliyojifunza kwenye barua hii.

Rafiki yako anayekupenda sana,

Kocha Dr. Makirita Amani,

www.amkamtanzania.com/kocha

0755 953 887 / kochamakirita@gmail.com

**MUHIMU;** KAMA HUJAPATA BARUA ZA NYUMA, FUNGUA; www.kisimachamaarifa.co.tz/barua2021